Motifu ya Utaifa katika Bunilizi za Kihistoria za Watoto za Mugyabuso Mlinzi Mulokozi: Ubainifu Wake, Sababu na Umuhimu wa Motifu Hiyo

L.H. Bakize
Chuo Kikuu cha Zimbabwe, Zimbabwe

Ikisiri

Wachambuzi mbalimbali wa fasihi wamekuwa wakisisitiza kwamba urudiaji unaojitokeza katika kazi mbalimbali za mwandishi mmoja husukumwa na nia ya mwandishi husika kutaka kusisitiza jambo fulani (taz. Okpewho, 1992; Ntarangwi, 2004;Senkoro, 2011). Hata hivyo, utafiti wa hivi karibuni uliofanywa na Kimbi (2016) katika kazi tatu za Mulokozi, unaonesha kwamba, tofauti na ilivyokuwa inachukuliwa hapo awali, urudiaji wa dhamira katika kazi za fasihi una dhima nyingi zaidi ya ile ya kusisitiza jambo. Utafiti wa Kimbi (2016) unabainisha kwamba Mulokozi alirudia dhamira ya uzalendo katika vitabu vyake vitatu, yaani *Ngoma ya Mianzi* (1991), *Ngome ya Mianzi* (1991) na *Moto wa Mianzi* (1996) kwa nia ya kuweka msisitizo, kukamilisha hadithi au kisa kilichopaswa kukamilika katika vitabu vyote vitatu, kuonyesha falsafa ya mwandishi, n.k. Bila kurudufu matokeo ya utafiti huo wa Kimbi, makala haya yanakusudia kuchambua motifu ya utaifa katika kazi nne za Mulokozi, yaani *Ngoma ya Mianzi* (1991), *Ngome ya Mianzi* (1991) *Moto wa Mianzi* (1996) na *Utenzi wa Nyakiiru Kibi* (1997). Kwanza makala inavichambua vitabu husika kwa kuangalia namna motifu ya utaifa inavyojitokeza. Pili, makala inatoa ufafanuzi wa kwa nini mwandishi aliamua kutumia motifu hiyo katika kazi zake. Mbali na uchambuzi wa vitabu teule, makala yametumia pia data za uwandani zilizopatikana kutoka katika mahojiano maalumu aliyoyafanya mwandishi wa makala na mwandishi wa vitabu teule. Makala yanaongozwa na mwega wa Nadharia ya Uoniafrika, ambayo hudai kwamba kazi za kifasihi za Kiafrika zinaweza kueleweka kwa usahihi zaidi kwa kujikita katika mazingira ya kijadi na historia ya jamii husika za Kiafrika. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kwamba kazi teule zilizochambuliwa zina maudhui muhimu yenye mchango mkubwa katika ujenzi wa dhana ya utaifa kwa watoto. Makala yanachambua motifu ya utaifa kwa kina na kisha kuonyesha thamani ya kazi teule katika kuwaandaa watoto wa Kitanzania kuipenda nchi yao na kuitumikia kwa moyo wa umoja.

Maneno Muhimu: Motifu, Motifu ya Utaifa, Bunilizi za Kihistoria za Watoto, Nadharia ya Uoniafrika

Utangulizi

Dhana ya motifu katika fasihi inafafanuliwa kuwa ni kipengele radidi cha kifani au kimaudhui kinachojirudia katika kazi za fasihi (Mulokozi, 1996). Wamitila (2003) anaeleza kwamba dhana hii hutumiwa kurejelea wazo kuu na sehemu ya dhamira katika kazi ya kifasihi. Nayo *Encyclopedia the Free Dictionary*[1]inaeleza kwamba motifu ni kitu, jambo, wazo au muundo katika kazi ya fasihi unaojirudiarudia. Aidha, Nyamsenda (2015) anabainisha kuwa motifu ni muhimu kwa sababu inamwezesha msomaji wa kazi ya fasihi kuona mawazo makuu na dhamira anazojaribu kuzionesha msanii ili msomaji aweze kuifasili na kuielewa kazi ya sanaa kwa ufasaha zaidi. Hivyo, motifu ya utaifa katika makala haya inarejelea hali ya kujirudiarudia kwa dhamira ya utaifa katika kazi teule zitakazochambuliwa.

Kabla ya kuangalia mambo mengine, ni vyema nifafanue kuhusu "taifa" na "utaifa." Maneno haya yanahusiana na kuingiliana katika matumizi ingawa sio visawe. Neno "taifa" linafasiliwa kama "jamii ya watu wanaoishi katika nchi moja na wanaounganika kutokana na matukio ya kihistoria; mfumo wa uchumi na utamaduni chini ya serikali moja" (TUKI, 2013: 534). Pia, chanzo kingine kinafafanua taifa kuwa ni "nchi inayochukuliwa kama kundi la watu wenye lugha moja, utamaduni na historia inayofanana, wanaoishi katika eneo fulani linalotawaliwa na serikali" (Oxford, 2015: 998). Maana zinazotokana na vyanzo hivi zinaonekana kufanana ingawa maana ya Oxford ina ukakasi kidogo. Ukakasi uko katika hoja ya watu wa taifa kuzungumza lugha inayofanana. Ukweli unaonesha kwamba kuna mataifa mengi tu ambayo watu wake wanazungumza lugha tofauti lakini bado wanajichukulia kuwa taifa moja. Hivyo, maana ya kwanza iliyotolewa na TUKI, ndiyo itakayotumika katika makala haya. Aidha, niongeze kwamba taifa linakuwa na jina ambalo huchukuliwa kuwa kama mwavuli unaowafunika na kuwakutanisha wanajamii husika. Kwa mfano, Tanzania ni nchi kijiografia lakini pia ni "taifa" kijamii. Watu wanaoishi nchini Tanzania, hujichukulia kuwa jamii moja pana yaani "taifa la Tanzania." Kwa upande mwingine, neno "utaifa" linamaanisha hali ya watu ambao hata kama wanaishi mbalimbali, na kuwa na tofauti ndogondogo, bado wanajichulia kuwa wa jamii moja pana iliyo chini ya serikali moja. Hali hii ndiyo iliyomsukuma Benedict Anderson kuchukulia taifa kama "Jamii ya Kufikirika" (Anderson, 2006). Kwa maelezo niliyotoa kuhusu taifa na utaifa, itoshe tu kusema kwamba taifa ni dhana pana inayomeza pia utaifa. Ndiyo maana utaifa unajengwa kwenye bongo za watu. Kwa hali hii, ujenzi wa utaifa ni ujenzi wa dhana mshikamano wa kitaifa katika bongo za watu (Nyerere, 1968). Kwa ujumla, makala haya yatajikita katika ujenzi wa utaifa ingawa hapa na pale dhana ya taifa nayo inaweza kugusiwa wakati wa ufafanuzi.

Fasihi ni zao la jamii na kwa ajili ya jamii. Hii ni sawa na kusema kuwa jamii huvyaza fasihi, nayo fasihi huiathiri jamii kwa hali chanya au hasi (Mshengyezi, 2003).

---

[1]https://www.thefreedictionary.com/motif

Memmi (2006) anasisitiza kuwa waandishi wa fasihi wana chombo muhimu sana mikononi mwao ambacho kutokana na ubunifu wao huwawezesha wasomaji kuamini na kuathiriwa na kile wanachokisoma au kusikiliza. Memmi (2006) anashadidia hoja yake kwamba hata kama kazi fulani ya fasihi ni ya kubuni, bado wahusika wake wanaweza kubebeshwa mawazo ya waandishi kuhusiana na jinsi ambavyo wasanii huyaona maisha na wanavyotamani maisha hayo yawe. Hivyo, yeye anahitimisha kwa kusema kuwa fasihi ni chanzo endelevu na cha muhimu katika ujenzi wa dhana ya utaifa. Aidha, Amuta (1989) anaeleza kwamba baada ya nchi nyingi za Kiafrika kupata uhuru, fasihi ya Kiafrika nayo imejikita katika suala la utaifa kwa kufukua matukio kadhaa muhimu ya kihistoria, uzoefu wa kijamii na mashujaa katika historia ya kitaifa na kuyafafanua mambo hayo kwa kutumia bunilizi za kifasihi. Lengo la uandishi wa mkondo huu ni kujenga urithi wa pamoja wa kihistoria ambao huwa nguzo muhimu katika kuwakumbusha watu walikotoka, walipo kwa muda husika na hivyo kuwahamasisha kuamua kuhusiana na mustakabli wa taifa lao. Historia ya taifa huiimarisha jamii husika kifikra, kimwelekeo, na katika kuwa na msimamo juu ya masuala mbalimbali ya kujenga jamii endelevu. Ujenzi wa taifa katika nchi yoyote ile, ni suala endelevu ambalo halina ukomo kutokana na changamoto na mabadiliko ya hapa na pale (Köksal, 2001). Hivyo, kila siku na kila wakati harakati mbalimbali zinaendelea kufanywa ili kuendeleza ujenzi wa taifa katika nchi zote.

Dhana ya utaifa katika kazi za fasihi imejadiliwa na watafiti mbalimbali ndani na nje ya Bara la Afrika kwa nyakati tofauti. Wengi wanaonekana kukubaliana kwamba fasihi ina nafasi kubwa katika ujenzi endelevu wa taifa (taz. Jacobs, 1952, 1961;Cianciolo, 1981; Chinweizu, 1987;Musiyiwa, 2008; Rycik &Rosier, 2009; Muwati, Gwekwerere & Gambahaya, 2010, kwa kutaja wachache). Kwa kuzingatia umuhimu huu, makala haya yanalenga kuchambua motifu hiyo ya utaifa ambayo imejitokeza katika kazi za watoto za M. M. Mulokozi. Nilivutiwa na kazi za mwandishi huyo mmoja kwa kuwa motifu hiyo imejirudia sana katika kazi zake zote nne, jambo ambalo ni la kipekee. Katika kuweka mtiririko mzuri wa hoja zangu, makala haya yatakuwa yakijibu maswali makubwa matatu. Mosi, "motifu ya utaifa imejitokeza vipi katika kazi za mwandishi teule?" Pili, "ni mambo gani yaliyomsukumu mwandishi kuirudia dhamira hii ya utaifa katika kazi zake zote nne?" Tatu, bunilizi za kihistoria za watoto zilizochambuliwa zina manufaa gani kwa watoto wanaozisoma kuhusiana na dhana ya utaifa? Katika sehemu inayofuata nitazungumzia kuhusu mbinu za utafiti zilizotumika katika kupata data za makala.

Mbinu za Utafiti na Kiunzi cha Nadharia

Makala haya yanatokana na utafiti wa maktabani na uwandani. Data zilipatikana kwa njia ya usomaji wa vitabu vinne vya watoto vilivyoandikwa na Mulokozi. Kazi zilizosomwa na kuchambuliwa ni*Ngoma ya Mianzi (1991), Ngome ya Mianzi (1991) Moto wa Mianzi (1996)* na *Utenzi wa Nyakiiru Kibi (1997).* Kama nilivyodokeza katika utangulizi wa makala haya, kazi za mwandishi teule ziliteuliwa kwa sababu ya kuwa na motifu ya utaifa. Dhamira hiyo imekuwa ikijirudiarudia katika vitabu vyote vinne ambavyo vimeandikwa na mwandishi mmoja. Urudiaji huu ulinivutia na kunifanya

nijiulize kwa nini mwandishi alifanya hivyo. Aidha, data nyingine ya makala haya ilitokana na mahojiano binafsi niliyoyafanya na mwandishi wa vitabu husika. Mahojiano hayo yalifanyika ofisini kwa mwandishi wa vitabu teule katika nyakati tofauti za mwezi Januari, 2017.

Makala haya yanaongozwa na nadharia ya Uoniafrika. Hii ni nadharia iliyoibuka baada ya nchi nyingi za Afrika kupata uhuru. Nadharia hii ilikita mizizi zaidi katika miaka ya 1970 na 1980 kutokana na Waafrika wengi, katika kona mbalimbali za dunia, kuona kwamba Mwafrika alikuwa anarejelewa kutokea pembeni. Mwafrika alikuwa anabezwa na mara nyingi akitathminiwa kwa kutumia vipimo au vigezo vya wazungu. Ndiyo maana mambo mengi ya Waafrika yalikuwa yanabezwa. Hoja kubwa ya nadharia hii ya Uoniafrika ni kumtazama na kumtathmini Mwafrika kwa kuzingatia historia yake na akiwa kwenye kiini cha utamaduni wake. Wafuasi wa nadharia hii wanatajwa kuwa ni pamoja na Chinua Achebe, Ngugi wa Thiong'o, Chinweizu, Okot p'Bitek, Molefi Kete Asante, miongoni mwa wengine. Inaelezwa kwamba uchambuzi wowote unaojikita katika utamaduni wa Kiafrika, uwe ni wa kifasihi au kiuchumi, uwe ni wa kisiasa au kiutamaduni, lazima ujali mtazamo unaojikita katika historia na utamaduni wa Mwafrika mwenyewe (Asante, 1998, 2003; Okafor, 2010).

Nadharia hii ina mikondo mingi ya mitazamo. Hata hivyo, mimi katika makala haya, nitaitumia Nadharia hii kwa kujikita katika wazo kwamba, fasihi ya Kiafrika ina jukumu kubwa la kulibadilisha taifa katika nyanja zake zote na kwa sababu hiyo, mwandishi anapaswa kujikita katika uandishi unaolenga kujenga taifa. Achebe (1976) na Chinweizu (1987) wanafafanua kwamba mwandishi wa Kiafrika anatakiwa kuwa kama mwalimu wa jamii ambaye anapaswa kuifundisha jamii kuhusu historia na utamaduni wake ili kuimarisha utamaduni wa jamii husika. Jukumu mojawapo la mwandishi kama mwalimu wa jamii ni kuikosoa jamii hata kama jamii hiyo itamgeuka na kutaka kumdhuru. Hivyo, kazi kubwa ya mwandishi ni kusimamia ukweli wa mambo ili kuibadilisha jamii (Achebe, 1976, 1990).

Muhtasari wa Kazi Teule

Kama nilivyodokeza hapo awali, makala haya yatajikita katika uchambuzi wa bunilizi nne za kihistoria za Mulokozi ambazo nimezitaja hapo juu. Kazi tatu za mwanzo za Mulokozi, yaani *Ngoma ya Mianzi*, *Ngom*e *ya Mianzi* na *Moto wa Mianzi,* zote zinasimulia kisa kimoja chenye mtiririko mrefu. Mwandishi mwenyewe anauita mtiririko huo, kuwa ni "mfululizo wa hadithi za "Mianzi" (*Moto wa Mianzi*, uk. iv). Hadithi zote tatu zinazokamilisha mfululizo wa hadithi za mianzi zinasimulia mapambano ya Wahehe na Wadachi kwenye miaka ya 1891-1898. *Ngoma ya Mianzi* inasimulia jinsi mapambano yalivyoanza kati ya Wahehe na Wadachi mwaka 1891. Riwaya ya *Ngome ya Mianzi* inaendeleza simulizi hiyo kwa kujikita katika kisa cha vita vya Lugalo vilivyopiganwa kati ya Wahehe na Wadachi waliovamia eneo la Wahehe mwaka 1891. "Katika vita hivyo, Wahehe wakiongozwa na Jemedari Mupangile ndugu ya Mutwa (Mfalme) Mkwawa, kwa mara ya kwanza walilishinda na kuliteketeza kabisa jeshi hasimu la Wadachi" (*Ngome ya Mianzi,* uk. vi). Katika *Moto wa Mianzi* simulizi inaendelea kwa kueleza matukio ya vita vya Kalenga vya mwaka

1894. Matukio hayo ya vita vya Kalenga ni pamoja na kuteketezwa kwa lipuli (ngome) ya Kalenga, kukimbia kwa *Mutwa* Mukwava, kutawazwa kwa Mupangile, kukamatwa na kupelekwa uhamishoni kwa Sapi. Kwa ujumla, matukio hayo ya mapambano kati ya Wahehe na Wadachi yaliacha kumbukumbu isiyofutika katika taifa la Tanzania. Matukio hayo hayasahauliki kwa sababu yanafunza watoto kuhusu ushujaa na uzalendo wa mababu zetu waliopigania nchi yao isivamiwe na mabeberu. Ingawa babu zetu walishindwa katika vita hivyo, pengine kutokana na uduni wa zana zao, lakini moyo wao wa umoja, upendo, uzalendo, utu, kujitoa muhanga, ushujaa, na kadhalika, havitasahaulika kamwe katika historia ya taifa la Tanzania.

Utenzi wa Nyakiiru Kibi unasimulia kuhusu matukio ya karne ya 15 katika kuanzishwa kwa utawala wa ukoo wa Babito katika himaya ya Kiziba katika wilaya ya sasa ya Bukoba. Kwa maelezo ya mwandishi mwenyewe (taz. kwenye dibaji), Babito walikuwa ni wahamiaji wa Kiluo kutoka Uganda ambao walifika Kiziba wakitokea Bunyoro nchini Uganda. Huko Uganda, kabla ya kuja Bukoba, walikuwa tayari ni watawala. Simulizi hii ya kusisimua, ambayo imeandikwa kwa mtindo wa utenzi, inatumia jamii ya Babito kusimulia maingiliano na ushirikiano mzuri uliokuwapo katika jamii mbalimbali katika kujenga taifa na ustawi wao. Katika maingiliano hayo, ambayo yanaunda dhana ya utaifa, hakukuwa na mambo ya ukabila wala ubaguzi. Hata kama mambo hayo ya ukabila yalijitokeza basi yalijitokeza kwa kiasi kidogo kwa sababu hayakuwa na nguvu kabisa ya kuweza kuwagawa watu. Nia ya mwandishi ni kuwafundisha vijana kuhusu historia ya jamii zao na jinsi watu walivyoishi kwa upendo na umoja katika kujenga taifa.

Uchambuzi na Uwasilishaji wa Data

Katika sehemu hii ninabainisha jinsi motifu ya utaifa inavyojitokeza katika kazi teule. Kama nilivyosema hapo awali, motifu hii ya utaifa imebainika baada ya kusoma kazi teule na kwa mujibu wa data zilizopatikana kutokana na mahojiano ambayo niliyafanya na mwandishi wa kazi teule. Baada ya kukusanya data za makala haya na kuichambua, yafuatavyo yamebainika kuijenga motifu ya utaifa katika kazi teule.

Umoja na Mshikamano kama Msingi wa Utaifa

Mwandishi wa kazi teule zilizochambuliwa amelionesha jambo la umoja na mshikamano kwa namna mbalimbali na kwa msisitizo. Katika *Ngoma ya Mianzi, Ngome ya Mianzi* na *Moto wa Mianzi* mwandishi ameijenga dhana ya umoja na mshikamano kwa namna mbalimbali zifuatazo:

Mosi, amesisitiza dhana hii kwa kuwatumia watoto Mbumi (msichana) na Chulu (mvulana) katika *Ngoma ya Mianzi* na Nyawelu (msichana) na Mugoha (mvulana) katika *Ngome ya Mianzi* na *Moto wa Mianzi*. Watoto hawa ambao wanatoka kwenye familia tofauti, ambazo ni majirani, wanakua katika umoja na mshikamano wa hali ya juu. Kwa mfano, mwandishi anawaelezea Mugoha na Nyawelu kwamba watoto hao waliishi kama mapacha ingawa hawakuzaliwa pamoja. Walishirikiana katika shida na raha na wala hawakuachana katika nyakati zote (taz. *Ngome ya Mianzi,* uk. 1). Katika *Moto wa Mianzi* (uk. vii), Mugoha anasema, "Ingawa Nyawelu na mimi hatukuzaliwa

tumbo moja, lakini maafa ya Lugalo yaliyotuacha bila wazazi, yalituunganisha kama kaka na dada na kutuachia kazi ya kumlea mdogo wetu yatima, Semuganga." Katika *Utenzi waNyakiiru Kibi*, mwandishi anaonyesha umoja na mshikamano kati ya Nyakiiru na Kanyamaishwa ambao walichanjiana undugu (kur. 46-47). Urafiki wao ulikuwa imara na wenye faida. Bila kuvunja umoja na mshikamano wao, waliamua kuanza harakati za kuwaokoa watawaliwa waliokuwa wanaonewa na kunyanyaswa na mfalme Ntumwa (kur. 85-87). Katika umoja huo, Nyakiiru na Kanyamaishwa walifanikiwa kumpindua Ntumwa na kuwakomboa watu ambao walikuwa wakiishi kwa hofu, mashaka, kuuliwa ovyo, kuonewa, na kadhalika.

Pili, katika *Ngoma ya Mianzi,* mwandishi ameitumia jamii ya Wahehe wa Iringa na ile ya WanaKw'iloza wa huko Usagara. Jamii hizi zilikuwa na umoja na mshikamano wa hali ya juu. Wahehe walishirikiana katika mambo mengi chini ya mtawala wao Mutwa Mukwava na wasaidizi wake, na wana Kw'iloza walishirikiana chini ya kiongozi wao Mundewa. Jamii hizi mbili zinaonyesha kwamba watu wake walishirikiana kwa kila hali hata wakati walipovamiwa na mabeberu (Wadachi). Kwa upande wa watu wa Kw'iloza hawakuonyesha upinzani mkubwa sana wa wazi. Lakini, Wahehe, kwa umoja wao, walipambana na Wadachi kwa miaka kadhaa kati ya miaka 1891-1898. Katika umoja na mshikamano wa kitaifa, shida ya mwanajamii mmoja inakuwa shida ya wote na adui wa taifa anakuwa adui wa jamii nzima.

Tatu, mshikamano kupitia kikundi cha ulinzi cha Sokomoko (huko Usagara) na kile cha Wanyigendo (huko Uhehe). Mwandishi anaeleza kwamba kikundi cha Sokomoko kilikuwa kikundi cha kisiri katika vijiji mbalimbali vya Usagara. Kikundi hiki kiliundwa na watoto na mkuu wake alikuwa na umri wa miaka kumi na minane (taz. *Ngoma ya Mianzi* uk. 4). Kikundi hiki kilifanya kazi kubwa ya kuwaghasi Waarabu wateka watumwa waliokuwa wakipita Kw'iloza huko Usagara. Wadachi walipoingia huko Usagara, kikundi hiki kilipewa jukumu kubwa la kupeleleza nyendo zao, kujua mipango yao, na kupeleka habari kuhusu mipango yao ya mapambano katika vijiji vya Usagara (taz. dibaji ya *Ngoma ya Mianzi*). Watoto wa kikundi cha Sokomoko walikuwa na nguvu kubwa ya umoja na mshikamano kwa hali ya juu katika kutekeleza majukumu ya ulinzi wa taifa lao. Wanasokomoko walikuwa wamoja, na walikuwa tayari kutumwa kokote kwa ajili ya usalama wa nchi (taz. *Ngoma ya Mianzi* uk. 8), watoto walikuwa tayari kufa kwa ajili ya nchi yao (*Ngoma ya Mianzi* uk. 27), walipokamatwa na kuteswa hawakuwa tayari kutoa siri (*Ngoma ya Mianzi* kur. 43-44). Sifa za umoja na mshikamano wa watoto hawa ndizo hizo hizo zinazojitokeza katika kikundi cha Wanyigendo wa jamii ya Kihehe katika *Ngome ya Mianzi* na *Moto wa Mianzi*.

Malezi ya Watoto

Katika *Ngoma ya Mianzi*, watoto Mbumi na Chulu wanachorwa kama watoto waliokulia katika mikono ya wanajamii wote. Katika *Ngome ya Mianzi*, *Moto wa Mianzi*, Mugoha na Nyawelu nao walikulia katika mikono ya wanajamii wote. Tangu utoto wao walionekana kukua wakiwa wanamilikiwa na jamii nzima. Hali kadhalika, katika *Utenzi wa Nyakiiru Kibi*, Kanyamaishwa, baada ya kutupwa na baba yake

mzazi, kwa hofu ya kupokonywa utawala, aliokotwa na mama mmoja. Mama huyo alimlea Kanyamaishwa kama mtoto wake ingawa hakumzaa. Baada ya mtoto kukua mama huyo akafa (kur. 26-27). Kanyamaishwa akaanza kujitegemea. Katika ujana wake ndipo alipokutana na Nyakiiru (uk. 42). Kutokana na ushujaa aliokuwa nao Kanyamaishwa, Nyakiiru alimpenda na hivyo wakaamua kuweka urafiki wa kuchanjiana damu (kur. 46-47). Urafiki huo ulikua imara na hatimaye wakaweka pamoja mpango wa kuliokoa taifa la Babito ambalo lilikuwa linaongozwa kidikteta na na mfalme Ntumwa (kur. 73-85). Nia ya Nyakiiru na Kanyamaishwa ilikuwa ni kumpindua Ntumwa na kuwaweka huru watawaliwa ambao walikuwa wanaishi kama watumwa katika nchi yao wenyewe (uk. 87).

Umuhimu wa Mashujaa katika Taifa

Katika *Ngoma ya Mianzi*, watoto Mbumi na Chulu wanaonyesha ushujaa wa hali ya juu. Hawakuwa na woga wowote katika kupambana na adui katika mazingira yoyote magumu kwa faida ya jamii yao. Walikuwa tayari kupambana na adui, kupambana na wanyama, njaa, uchovu na kadhalika ili kuhakikisha kwamba jamii yao inabaki salama (taz. *Ngoma ya Mianzi* kur. 8, 61-66). Kikundi cha Sokomoko ambacho kiliundwa na watoto wa rika tofauti kilionesha ushujaa wa hali ya juu. Wanasokomoko walikuwa tayari kumkabili adui bila woga (taz. *Ngoma ya Mianzi* kur. 27, 43, 44 & 61).

Hali kadhalika, katika *Ngome ya Mianzi* na *Moto wa Mianzi*, watoto Mugoha na Nyawelu wanaonyesha ushujaa wa hali ya juu. Walikuwa tayari kupambana na Mdachi wakati wowote, walikuwa tayari kukabiliana na njaa ya porini pamoja na wanyama wakali bila woga (taz. *Ngome ya Mianzi,* kur. 5-9, 16-18, 25-29, 36, 46-47). Kikundi cha wanyigendo nacho kilikuwa kama kile cha Sokomoko katika *Ngoma ya Mianzi*. Kikundi hiki cha wanyigendo kilikuwa na watu jasili sana kwa ajili ya jamii ya Wahehe. Kikundi hiki cha kizalendo kiliongozwa na Jemadari Mpunza. Jemadari huyu aliweka historia kwa kumuua kwa mkuki adui hatari sana wa Wahehe aliyejulikana kwa jina maarufu la Nyundo (Von Zelewisky). Huyu aliyeuawa alikuwa ni kamanda wa jeshi la Kidachi lililokuwa likipigana na Wahehe. Wanyigendo hawa walipeleleza nyendo za adui bila woga, walikabiliana na adui kwa ushirikiano, na pale ilipowezekana walimshinda adui huyo (taz. *Moto wa Mianzi,* kur. 10, 13, 30, 72, 85-87). Mashujaa wengine katika *Moto wa Mianzi* ni kama Sapi, Mupangile na Tovi. Ushujaa wao ulikuwa kwa faida ya jamii nzima na vizazi vijavyo.

Katika *Utenzi wa Nyakiiru Kibi* ushujaa unaendelea kujitokeza. Kutokana na ushaujaa wake, Kanyamaishwa anapata rafiki Nyakiiru. Walipopimama wote walijikuta kuwa wana sifa ya ushujaa unaolingana (uk. 42). Ushujaa wao unadhihirika zaidi wakati wakiwinda kandokando yaa ziwa Victoria. Nyakiiru alivamiwa na chui na Kanyamaishwa akamsaidia kumshinda chui huyo (kur. 48-51). Ushujaa wao (Kanyamaishwa na Nyakiiru) uliwasukuma hata kuamua kumpindua mfalme Ntumwa ambaye alikuwa anawatesa na kuwanyanyasa watu wa utawala wake (uk. 85). Kitendo hiki kilileta ukombozi kwa taifa la Babito ambalo lilitawaliwa kidhalimu na Ntumwa. Hatimaye, Nyakiiru na Kamyamaishwa walianzisha utawala mzuri wenye kupendwa na watu wao kutokana na upendo waliokuwa nao kwa jamii (uk. 87).

Umuhimu wa Historia ya Jamii kwa Watoto

Katika *Ngome ya Mianzi*, mhusika bibi anamfunza Mugoha historia ya jamii ya Wahehe. Bibi alimsimulia historia ya ushindi na ushujaa wa wazee wa Uhehe ili kumfanya Mugoha ajione kuwa naye anaungana na mashujaa wa zamani wa jamii yake ambao walipambana katika kulinda nchi yao. Bibi alimsimulia habari za mashujaa wa zamani kama Muyinga, Munyigumba na Luhota na jinsi Mukwava alivyopambana na Waarabu wateka watumwa na kuwashinda (uk. 26). Pia, katika *Utenzi wa Nyakiiru Kibi*, Mulokozi anasisitiza umuhimu wa historia na urithi wa jamii. Katika tabaruku ya kitabu hicho, mwandishi anadai kuwa kitabu hicho kimeandikwa kwa ajili wa wana wa nchi ya Tanzania ambao wengi hawajui mambo ya kwao kihistoria. Anabainisha kwamba kujua mambo ya wahenga wa jamii ni muhimu kwa sababu ndio urithi na tunu ya jamii (taifa). Tena anawaasa watoto kwamba wasome mambo hayo ya historia ya jamii zao kwa kuwashirikisha hata wale wasiojua kusoma. Kwa kuwa mambo hayo ya urithi wa taifa ni muhimu, basi wasomaji wanaaswa kwamba wanapomaliza kuyasoma basi wayahifadhi kwa ajili ya vizazi vijavyo (taz. tabaruku ya kitabu). Mwandishi anasisitiza pia mambo hayo ya historia ya jamii na urithi wa taifa katika ukurasa wa 1 na 2.

Mahusiano ya Kijinsia na Dhana ya Utaifa

Mwandishi anaibua jambo jingine la kijamii (kitaifa) ambalo ni muhimu katika masuala ya utaifa. Jambo hilo ni mahusiano ya kijinsia. Mahusiano ya kijinsia yameonyeshwa katika sura ya uwili. Kwa upande mmoja, mwandishi ameonyesha kwamba kutokana na mfumodume wa kijamii, mtoto wa kike (kwa kuwakilisha wanawake) ana mipaka yake kiutendaji. Yapo majukumu ambayo ni ya kike na mengine ni ya kiume. Hata uwezo wa kupambana na mambo magumu, unahusishwa zaidi na mvulana. Katika *Moto wa Mianzi*, Nyawelu anapowaambia Sapi na Mugoha kwamba naye atashika zamu ya kulinda usiku, Sapi anashangaa na kuona kuwa ni jambo lisilowezekana. Mwandishi anatueleza kwamba ingawa Sapi aliapa kutoruhusu Nyawelu ashike jukumu la kushika zamu ya ulinzi, lakini usiku ulipofika Nyawelu aliwalinda vizuri wao wakiwa hawajitambui kutokana na usingizi. Kesho yake, Mugoha na Sapi walipoamka, Nyawelu aliwataarifu kuwa aliimarisha ulinzi usiku wakati wao wakiwa wamelala. Kitendo hicho kiliwashtua na kuwashangaza sana kwa sababu hakikutarajiwa kufanywa na mwanamke (uk. 27).

Kwa upande wa pili, mwandishi anaonekana kufanya mapinduzi kijamii. Ingawa mwandishi anafahamu kwamba kuna suala la mfumodume katika jamii, yeye anaamua kupingana na jamii kwa kufanya utafiti na kumweka mwanamke kwenye maabara ya utendaji. Mwandishi anaonekana kujenga ulimwengu wake ambao ni tofauti na ule uliozoeleka. Mwandishi anaamua kumweka msichana katika mazingira yote magumu ili kuionyesha jamii kuwa mawazo mgando yaliyopo kuhusu uwezo wa mwanamke siyo sahihi. Katika *Ngoma ya Mianzi*, Mbumi anaonekana kuwa na uwezo mkubwa kumzidi hata Chulu. Kwa mfano, Mbumi anaonekana kuwa mwepesi kuhisi mazingira ya hatari (uk. 3), ni mwepesi kutoa mawazo ya kibunifu wakati wa hatari (kur. 3, 14, 20, 32 na 33), alikaa tayari muda wote kukabiliana na adui kivita (uk. 34), alikuwa

mkali kwa adui, alikuwa mjanja na jasiri ambaye hakuogopa hata kifo kwa ajili ya taifa lake (uk. 37). Mathalani, katika ujasiri, aliweza kumwokoa Chulu aliyekuwa ametekwa na Wadachi. Alitumia mbinu za ajabu kwa kuiendea kambi ya Wadachi usiku mpaka akamkomboa Chulu (kur. 38-42). Alijitoa mhanga kwa kuwaporomshea mawe Wadachi na kuwaua wengi (uk. 58). Mbumi alikuwa ameapa na akasisitiza kwamba hata iweje, hataweza kutoa siri kuhusiana na taifa lake (uk. 61). Mwisho, Mbumi alibuni mbinu ya hatari kwa kumlevya askari wa Kidachi kisha akamkamata na kumfunga na askari akawa mateka wake (kur. 61-63).

Katika *Ngome ya Mianzi* na *Moto wa Mianzi*, Mulokozi anaendeleza wazo lake la kumfanya mwanamke shujaa. Nyawelu anaonekana kuwa na akili nyingi na shujaa kama Mbuni wa *Ngoma ya Mianzi*. Katika *Ngome ya Mianzi* Nyawelu alikuwa na uwezo mkubwa sana kiasi kwamba hata Mugoha mwenyewe alikiri kuwa Nyawelu alikuwa shujaa kumzidi yeye (uk. 5). Katika nyakati za hatari, Nyawelu anaonekana kuwa na uwezo mkubwa wa kufikiri na kuwaokoa wenzake kabla hawajaingia hatarini (kur. 18, 36, 46 na 47). Ujasiri na uwezo wa Nyamwelu unamshangaza Mugoha. Mugoha anakiri mbele ya Bibi kwamba Nyawelu ni msichana jasiri na wa pekee sana. Bibi anamjibu "tabia ya kweli ya mtu utaijua wakati wa dharura" (uk. 26). Ushujaa wa Nyawelu bado unajitokeza pia katika *Moto wa Mianzi*. Bado anaonekana kuwa askari shujaa (uk. 10). Mugoha mwenyewe anaendelea kukiri kuwa Nyawelu alikuwa shujaa kwa kusema "Nyawelu alikuwa ni msichana wa ajabu. Alikuwa mvumilivu, mkomavu na jasiri. Aliweza kustahimili wakati sisi tuliojiita wanaume tulipoporomoka kama vifusi kwa uchovu. Niliona fahari iliyochanganyikana na aibu-fahari ya kuwa ndugu wa msichana kama huyu; aibu ya kushindwa kutimiza wajibu" (uk. 27). Sifa nyingine za ushujaa wa Nyawelu zinabainishwa katika kurasa za 31, 51, 64, 65 na 70.

Mwandishi kwa namna nyingine, ameamua kumwinua mwanamke kwa kumtumia mhusika bibi katika *Ngoma ya Mianzi*, *Ngome ya Mianzi* na *Moto wa Mianzi* na mhusika mama katika *Utenzi wa Nyakiiru Kibi*. Tangu katika kitabu cha *Ngoma ya Mianzi*, *Ngome ya Mianzi* na *Moto wa Mianzi*, bibi anaonekana kushika nafasi kubwa sana ya ulezi na kuwaelekeza Nyawelu na Mugoha namna ya kupambana na maisha. Nafasi ya mwanamke kama mlezi muhimu wa watoto linajitokeza pia katika *Utenzi wa Nyakiiru Kibi*.

Chuki kwa Adui wa Taifa

Katika vitabu vyote teule vinne, dhana ya chuki kwa adui wa taifa inajitokeza. Mwandishi anaonyesha kwamba ili watoto wakue wakiwa na wazo la utaifa vichwani mwao, kuna umuhimu wa kuwapa moyo wa uzalendo na kuwapandikiza chuki dhidi ya adui wa taifa lao. Mwandishi kwa maksudi anapandikiza chuki kwa wasomaji dhidi ya utumwa, ukoloni na wizi wa mali ya umma. Katika *Ngoma ya Mianzi* mwandishi anaibua suala la chuki dhidi ya utumwa kwa kuonyesha jinsi kikundi cha sokomoko kilivyokuwa kinawaghasi Waarabu waliokuwa wanateka watumwa na kwenda kuwauza huko Pwani ya Tanzania. Mbumi na Chulu walikuwa na hasira sana dhidi ya Waarabu ambao walimchukua mama yao na kumpeleka huko Bagamoyo kama mtumwa (taz. dibaji). Kikundi cha sokomoko kiliwachukia sana Waarabu kwa sababu

ya biashara ya watumwa. Biashara hiyo ya watumwa iliacha familia zikiwa zimesambaratika, hazina amani, watoto walikosa malezi, na kadhalika. Hivyo, chuki dhidi ya utumwa iliwafanya wanasokomoko wamchukie Mwaraba na kuwa tayari kupambana naye kisirisiri. Katika *Ngome ya Mianzi*, mwandishi anawatia hasira watoto kupitia unyama na ukatili uliofanywa na wakoloni. Mhusika Bibi anawasimulia Mugoha na Nyawelu juu ya uovu wa Wadachi na jinsi ambavyo hawakuwa na huruma na pia anawaarifu juu ya azma yao kwa nchi ya Wahehe (uk. 20). Anaeleza kwamba Wadachi ni watu wabaya sana. Nukuu ifuatayo inadokeza hoja yangu:

> "Wadachi ndio watu gani?" Nyawelu aliuliza.
>
> "Ni wazungu watoka mbali, wanangu. Watu wekundu, wauaji na makatili."
>
> "Wanakuja kufanya nini?" Niliuliza.
>
> "Kuchukua nchi. Kutugeuza watumwa."
>
> "Nchi wataipeleka wapi? Si wachukue ng'ombe…?"
>
> "Hawa hawaji kupora na kuondoka, wanakuja kukaa na kutawala." (*Ngome ya Mianzi*, uk. 20).

Aidha, katika kukoleza chuki dhidi ya adui wa taifa, mwandishi ameamua kutumia dhana ya wezi akiwarejelea wakoloni na wengine wote wanaochukua mali za umma bila uhalali. Katika *Moto wa Mianzi*, wandishi anahoji "Kwa nini watu wengi hapa Afrika ni wezi? Kama si wezi, basi wana tabia ya kutukuza wezi na bila shaka baadhi yao wangependa kuwa wezi kama wangepewa nafasi (uk. vi). Suala la wezi pia linatajwa katika kurasa za 18, 19, 20, 31, 34, 35, 66 na 69. Wezi wanaorejelewa na mwandishi ni Waarabu waliokuwa wanaiba mali za taifa na kuwachukua watumwa, wakoloni waliokuwa wanaiba rasilimali za umaa na kuwatumikisha watu kikatili, na wananchi wenyewe ambao wameambukizwa tabia mbaya ya wizi wa mali za taifa. Hao wote wanajumuishwa katika dhana ya wezi wa mali ya umma.

Dhana ya wezi inajitokeza tena katika *Utenzi wa Nyakiiru Kibi*. Ingawa mwandishi hakutaja suala la wezi moja kwa moja, lakini anawarejelea wazungu (wakoloni) kama watu wenye uroho au ulafi. Hawashibi hata wale nini. Sifa hiyo ilibainishwa kupitia mhusika Mutalala ambaye naye alikuwa Mwafrika mwenye sifa hiyo ya uroho.

Mwandishi katika ukurasa wa 72 anasema:

691	692
Dunia ina mizungu Imewazuia wazungu Na Mutalala mwenzangu Yu mzungu nakwambia.	Mzungu hawezi shiba Japo angemeza mamba! Nguruwe katika shamba Zimwi katika dunia.

Umuhimu wa Moyo wa Uzalendo wa Kitaifa

Uzalendo ya kitaifa unaonekana kusisitizwa kwa kurudiwa katika kazi zote nne zilizochambuliwa. Naye mwandishi, katika mahojiano, alikiri kuwa alifanya maksudi kusisitiza dhana hii ili atekeleze nia yake katika uandishi. Katika *Ngoma ya Mianzi*,

mwandishi ameonyesha kwamba watoto Mbumi, Chulu, Mpunza na wanasokomoko wote walikuwa wazalendo wa hali ya juu kwa jamii yao. Kwa mfano, katika ukura 27, Mbumi anasema, "ikibidi afadhali tufe kuliko kufichua siri ya nchi." Ukweli wa kauli ya Mbumi ulidhihirika pale Chulu alipokamatwa na Wadachi. Chulu alipigwa na kuteswa kwa kila namna lakini hakuwa tayari kutoa siri za nchi yake (kur. 44-45). Naye Mbumi akiwa katika hatari kubwa, wakati akikabiliana na askari wa Kidachi, alikwepa kijanja kutoa majibu ya maswali ya Mdachi ili kuhakikisha kwamba anabaki mzalendo wa taifa lake. Alikuwa tayari kufa na hakutoa siri kwa adui (uk. 61). Kutokana na uzalendo wa Waafrika, Wahehe waliweza kuwashinda Wadachi katika vita vya Lugalo mwaka 1891. Bila woga wowote, Wahehe walijitoa mhanga kwa nchi yao, kwa kupigana na mzungu mwenye bunduki na mabomu na silaha nzito ilhali wao wakitumia zana duni kama upinde na mishale, sime, mawe, manati, mapanga na mitego ya wanyama. Ingawa silaha hizo za Wahehe zilikuwa dhaifu lakini silaha yao kuu ya umoja na uzalendo vilikuwa imara.

Katika *Ngome ya Mianzi* uzalendo wa kitaifa unasisitizwa. Katika harakati za kupambana na adui (Mdachi) wa nchi ya uhehe, baba yake Mugoha alivamiwa na askari na kumjeruhi vibaya sana. Wakati anakaribia kukata roho, alimuusia Mugoha "Nimekusikia. Ahsante kwa kaz-inzu-nzuri uliyofafa-nya mwa-na-ngu. Mimi ni-na-na-kufa. Msai-idi-di-e ma-ma yako. Mle-e-e m-to-to-to ata-kaye-az-zaliwa. Ipi-ga-ni-e-nchi ya-ako." (uk. 31). Uzalendo unaenda sambamba na kitendo cha utayari wa kujitoa mhanga. Nchi inapovamiwa na adui, lazima wawepo wazalendo wa kujitoa mhanga kwa ajili ya wengine. Hali hii ndiyo inayoonekana katika vita hivi kati ya Wahehe na Wadachi. Wazazi na wanajamii mara zote waliwatia moyo wapiganaji kuwa wasife moyo na wala wasirudi nyuma kwa sababu wamebeba roho za watu wengi mabegani mwao. Ingawa mama yake Mugoha alikuwa taabani kitandani, alituma ujumbe kwa Mugoha aliyekuwa vitani kupitia Nyawelu. Nyawelu anasema "Lakini ameniagiza nikuambie upige moyo konde, kwani hukubeba roho yako tu, bali umebeba roho za maelfu ya watu. Anasema unayofanya sasa ni kwa ajili ya nchi hii" (uk. 33).

Dhana ya uzalendo bado inasawiriwa tena katika *Moto wa Mianzi*. Mugoha, Nyawelu na Wanyigendo bado wanapigania nchi yao bila hofu yoyote (uk. vii). Hata hivyo, mwandishi anatuonyesha upande wa pili kwamba katika vita vya kupigania nchi lazima kuwa makini kutokana na uwezekano wa kuwapo wasaliti wa taifa. Mhusika Kafugwa amesawiriwa kulisimamia jambo hili. Kafugwa anawasaliti Wanyigendo wenzake kwa kutoa siri kwa adui na hali hiyo inawaweka wenzake katika hali ngumu zaidi (kur. vii, 50, 51). Kafugwa mwenyewe baadaye alikiri kuwa aliwasaliti wenzake (uk. 53).

Usaliti ni adui mkubwa sana wa usalama wa nchi. Pia, mwadishi anamtumia mhusika Tovi na Mutwa Mupangile (kaka yake Mutwa Mukwawa) kuonyesha kwamba katika uzalendo wa nchi lazima wawepo watu wa kujitoa mhanga kupeleleza nyendo na utendaji wa adui ili iwe rahisi kummaliza adui (uk. 9). Kutokana na upepelezi huu, tena wa kushirikiana na adui, Tovi anafanikiwa kuiba punda (Sebu) kwa ajili ya harakati za kupigania nchi ya Uhehe. Mutwa Mupangile naye alijitoa kumtumikia

Mdachi kama mtumishi wakati huo akawa anakusanya taarifa za kummaliza adui. Kwa bahati mbaya Mutwa Mupangile aligundulika. Hata hivyo, alipokuwa anakaribia kunyongwa alitoa maneno mazito yenye wosia kwa wanyigendo wengine. Anasema:

> Kesho tutakufa. Lakini hilo si jambo kuu wala la kushangaza. Jambo muhimu ni kwamba hatufi kwa sababu ya ukongwe, au uhaini au ulafi, au hata kwa kuumwa na mbu. Hatuuawi kwa sababu tu wasaliti au waoga au majambazi. Tunakufa kwa sababu nchi yetu inahitaji muhanga wetu. Tunakufa wachache ili wengi wapone. Huo ndio upekee na ndiyo fahari ya kifo chetu (uk. 90).

Pia, ni kutokana na uzalendo tunamuona Tovi, ambaye aliiba punda wa Bruda, alipogundulika na kuteswa sana ili aseme punda alipo, anakubali kufa kuliko kutoa siri muhimu ya wanyigendo. Alikuwa tayari kufa bila kuisaliti nchi yake (uk. 30).

Mwandishi anaonyesha uzalendo wa kitaifa pia katika *Utenzi wa Nyakiiru Kibi*. Mwandishi anamuonyesha mfalme Ntumwa jinsi alivyokuwa mtawala mbaya na mdhalimu. Huyu alimuua mtawala mwenyeji na akajitwalia utawala kwa mabavu (uk. 6). Alikuwa kiongozi ambaye hata akiona mwanamke mzuri, basi kama alikuwa ameolewa, aliweza kumuua mume wake ili yeye amchukue (uk. 71). Mfalme huyu alinyang'anya hata mashamba ya maskini (uk. 72). Huyu hakuwa mzalendo hata kidogo. Kutokana na hali hii Kanyamaishwa na Nyakiiru waliamua kuonyesha uzalendo kwa wananchi, wakaamua kumpindua mfalme Ntumwa. Mapinduzi hayo yalifurahiwa sana na wananchi kwa sababu wananchi walibaki huru, waliishi kwa amani na upendo na kuongozwa vizuri na Nyakiiru Kibi (kur. 73-87).

Madhara ya Vita kwa Jamii na Taifa

Ingawa Mulokozi anaonesha ushujaa wa watoto na Waafrika katika mapambano ya kivita dhidi ya adui (Mwarabu na Mdachi), lakini anatahadharisha kwamba vita ni vibaya sana. Anaonesha msimamo huo kwa kuweka wazi madhara ya vita kwa jamii. Vita inapotokea huleta taharuki kubwa. Watu hukimbia huku na huko wa wakitafuta kujiokoa. Wanyama na ndege wa kufugwa nao huangamia na wengine hukimbia ovyo bila uangalizi wowote (taz. *Ngoma ya Mianzi* uk. 4). Katika *Ngome ya Mianzi*, mwandishi anaendelea kuonyesha madhara ya vita. Kwa mfano, kutokana na vita, vijana wawili (Mugoha na Nyawelu) walijikuta katika msukosuko mkubwa. Katika hali hiyo watoto hawa ilibidi wauache utoto wao kando na kubeba majukumu ya watu wazima ili kujinusuru na kuihami nchi yao bila hiari yao (uk. vi).

Madhara ya vita yanaonekana pia katika *Moto wa Mianzi*. Mwandishi bado anaweka msisitizo kwamba vita vyovyote vinaacha madhara makubwa kwa watu binafsi, familia, mazingira, na taifa kwa ujumla. Mwandishi anaeleza:

> Watoto waliachwa bila wazazi, wasichana waliachwa bila wachumba, na nchi iliachwa bila *mutwa*. Kwa kweli wakati huo watoto hawakupata nafasi ya kuwa watoto, na vijana walizeeka kabla ya kupevuka. Niliona vikongwe vikibebeshwa mitumba, na maajuza wakishika silaha kwenda vitani. Niliona wazee wa baraza la Uhehe walioheshimiwa na kila mtu wakilazwa chini na

> kuchapwa bakora ishirini na tano kwa amri ya kijana mdogo wa Kidachi (uk. vii).

Vita kati ya Wahehe na Wadachi, hasa baada ya pambano la Lugalo la mwaka 1891 ilisababisha maafa makubwa. Baada ya Wadachi kwenda kujipanga upya na kurudi, vita vya mwaka 1894 viliacha ikulu ya Mukwava ikiwa imeunguzwa yote, maiti za watu waliouawa zikiwa zimetapakaa, mazao yakiwa yameunguzwa, mifugo ikiwa imesambaratika, na kadhalika (kur. 6-10).

Nafasi ya Watoto katika Taifa

Tofauti na msemo uliozoeleka katika jamii za Waswahili kwamba “mtoto ni taifa la kesho,” mwandishi wa kazi teule yeye anaamini kwamba “mtoto ni taifa la leo na kesho.” Ikiwa mtoto ni taifa la kesho, maana yake leo anaandaliwa tu kwa ajili ya kesho. Mwandishi anaonekana kupingana na msemo huu. Yeye amemuweka mtoto katika kitovu cha maisha. Katika mazingira hayo, misukosuko ya maisha haichagui mtoto wala mtu mzima. Wote hujikuta kwenye uwanja wa mapambano. Hapo kila mmoja bila kujali kuwa ana umri au hadhi gani katika jamii, anajikuta ni mtendaji kwa namna mbalimbali, iwe ni kwa kupenda au kutopenda. Kama anavyosema mwandishi, wakati wa misukosuko ya kijamii, watoto hulazimika kukua kabla ya wakati. Hata watoto wenyewe wanapoitwa watoto hukana hadhi hiyo kutokana na mambo makubwa ambayo wamekabiliana nayo. Mugoha na Nyawelu wanapoulizwa kama wataweza kwenda Masombe kumleta mkunga wa kumzalisha mama Mugoha, Mugoha anajibu “kwa nini tusiweze, kwani sisi ni watoto wadogo?” (*Ngome ya Mianzi*, uk. 6).

Ni katika mazingira ya hatari ambapo tunamwona baba yake Mugoha akimwusia mwanawe kwamba “kukua ni kulikabili zimwi lenye vichwa kumi na kuvikata kimoja baada ya kingine bila kutishika. Ni kufuta machozi yako na ya wenzako. Ni utu uzima, ni kazi, ni majukumu” (taz. *Ngome ya Mianzi*, uk. 7). Hii inaashiria kwamba ingawa Mugoha na watoto wenzake walikuwa watoto lakini mazingira yatawakuza kwa lazima.

Kutumia wingi wa Makabila kwa Faida ya Umoja wa Kitaifa

Mwandishi anaonesha kwamba wingi wa makabila katika ujenzi wa taifa una faida kubwa. Badala ya kila kabila au jamii kupambana na adui peke yake, mwandishi anaonyesha kwamba makabila yakipendana na kuungana yanaweza kupiga hatua nyingi zaidi kimaendeleo. Hata anapotokea adui inakuwa rahisi kukabiliana naye na kumshinda. Baada ya Mukwava kuvamiwa na Wadachi, ingawa alikuwa na nguvu, aliona kwamba silaha nzuri ya kuwashinda ni ile ya kutumia nguvu ya umoja na mshikamano. Hivyo, aliamua kutuma ujumbe kwa mtawala ya Usagara ili waungane katika kumwondosha Mdachi (*Ngoma ya Mianzi*, uk. 7). Mundewa baada ya kupokea ujumbe kutoka kwa Mutwa Mukwava, aliafiki ombi hilo na hivyo akawaagiza akina Mbumi na Chulu wapeleke ujumbe kwa Mutwa kwamba Kw’iloza iko tayari kushirikiana na Uhehe katika vita vya pamoja vya kumng’oa Mdachi (*Ngoma ya Mianzi*, uk. 9-12).

Sababu za Mwandishi kutumia Motifu ya Utaifa

Katika kipengele kilichopita, nimebainisha vijenzi vya motifu ya utaifa inavyojitokeza katika bunilizi za kihistoria za Mulokozi. Baada ya kubainisha vijenzi hivyo, katika sehemu itakayofuata, nitajaribu kueleza sababu za mwandishi kutumia motifu hiyo ya utaifa katika kazi zake zote nne. Data za utafiti wa makala haya zinashawishi kwamba mwandishi alijikuta akiendeleza motifu ya utaifa katika kazi zake nne kwa sababu zifuatazo:

Kupunguza Pengo la Uhaba wa Bunilizi za Kihistoria katika Fasihi ya Kiswahili

Mulokozi alieleza kwamba bunilizi za kihistoria katika fasihi ya Kiswahili bado ni chache na zinahesabika. Kutokana na ukweli huu, wakati wa mahojiano, Mulokozi alieleza kwamba baada ya kuona pengo kubwa lililopo katika fasihi ya Kiswahili, hasa katika bunilizi za kihistoria, aliamua kuandika kazi za watoto za kihistoria kwa maksudi ili apunguze pengo lililokuwapo. Mukokozi alibainisha kwamba ingawa fasihi ya Kiswahili ya watu wazima ilikuwa na bunilizi walau chache za kihistoria, kwa upande wa fasihi ya watoto hali ilikuwa mbaya sana. Kwa hiyo, hali hiyo ilimsukuma kutoa mchango kwa kuandika *Ngoma ya Mianzi* (1991), *Ngome ya Mianzi* (1991), *Moto wa Mianzi* (1996) na *Utenzi wa Nyakiiru Kibi* (1997). Mwandishi anaeleza kwamba aliona akiandika vitabu hivyo atakuwa ametoa mchango mzuri katika kukomaza bunilizi za kihistoria katika fasihi ya Kiswahili. Zaidi, mwandishi anaeleza kwamba motifu ya utaifa ilikuwa muhimu katika kuongoza kazi zake kwa sababu ndiyo inayolengwa zaidi katika bunilizi za kihistoria za Tanzania hasa zinazowalenga watoto.

Kuunga Mkono Juhudi za Serikali katika Ujenzi wa Dhana ya Utaifa

Wakati wa mahojiano mwandishi wa kazi teule alisisitiza kwamba kitu kilichomsukuma kuandika bunilizi hizo za kihistoria ni kutaka kuunga mkono juhudi za serikali ya TANU [*Tanganyika African National Union*] katika ujenzi wa dhana ya utaifa. Mwandishi alidai kwamba kila serikali ina msimamo wake na namna inavyoendelea kujenga dhana ya utaifa. Wakati anaandika bunilizi hizo, ambazo utafiti wake ulianza miaka ya 1960, yeye alikuwa mwanachama wa TANU. Kwa maelezo yake, alikubaliana kwa kiasi kikubwa na falsafa ya ujenzi wa dhana ya utaifa iliyokuwa ikihubiriwa na serikali ya TANU ya kipindi hicho. Mulokozi alisema:

> Wakati wa Nyerere, miaka ya 1960, utawala wake ulikuwa unasukuma utaifa sana. Mpaka shuleni tulikuwa tunalazimika kucheza ngoma zetu. Tukaimba nyimbo za kusifu chama na Tanzania. Hata mafundisho ya historia tukaanza kufundishwa tofauti. Tukawa na mtazamo tofauti na ule wa kikoloni, tukaanza kufikiri kijadi, yaani Kitanzania. Hata mambo ya Mukwava tulifundishwa shuleni katika historia. Nakumbuka kabisa mambo ya vita vya MajiMaji.

> Mwanzoni, wazungu walikuwa wanafundisha kwamba wapiganaji wa Maji Maji walikuwa waasi, sasa tulipojifunza sisi tukaanza kuwaona kama waleta ukombozi. Walikuwa ni watetezi wa nchi, walikuwa ni wapigania uhuru, n.k. Kwa hiyo, serikali ya wakati huo ilikuwa inasisitiza uzalendo...[2]

Kuendeleza Kazi Binafsi za Utafiti

Uchambuzi wa data zetu za utafiti umeonesha kwamba Mulokozi alikuwa na raghba ya utafiti na uandishi wa mambo ya kihistoria kwa muda mrefu. Katika mahojiano Mulokozi alikiri kwamba ana uzoefu wa muda mrefu wa utafiti na uandishi wa mambo ya kihistoria yenye utaifa kwa njia ya sanaa. Hivyo, uandishi wa kazi zote nne ni matokeo ya mwendelezo wa harakati hizo za utafiti na uandishi wa kazi za bunilizi za kihistoria zenye mwelekeo wa kitaifa. Alisema:

> ….nilikuwa nimeshaanza kuandika mambo ya kihistoria kwa sababu hata tamthilia yangu ya *Mkwava wa Uhehe* niliiandika mwaka 1968. Kwa hiyo, nilikuwa na uzoefu mkubwa. Aidha, nilikuwa na upenzi na utafiti na uandishi wa vitabu vya kihistoria tangu zamani. *Utenzi wa Nyakiiru Kibi* vilevile ni wa kihistoria. Hata riwaya za *Ngoma ya Mianzi*, *Ngome ya Mianzi* na *Moto wa Mianzi* nazo zinafuata mkondo huohuo. Sababu mojawapo ya kuandika kwa mkondo huo ni kwamba niliamini kuwa ni muhimu watu wajitambue, wajijue hasa vijana na watoto wajue walikotoka. Hata ukiangalia utafiti wangu wa Uzamivu utaona kwamba unahusu Nanga, na tendi zake ni za kihistoria...[3]

Mwandishi anakiri kuwa uandishi wake wa *Ngoma ya Mianzi*, *Ngome ya Mianzi*, *Moto wa Mianzi* na *Utenzi wa Nyakiiru Kibi* ulitokana na tafiti mbalimbali alizokuwa akifanya kwa muda mrefu kuhusu jamii za Kitanzania. Nia ya kufanya utafiti huo ilikuwa ni kwa ajili ya jamii nzima kupata maarifa na elimu ya mambo ya zamani ili kuwezesha watu kujitambua, kujithamini kutokana na utajiri wa mambo yao ya zamani.

Msukumo Binafsi wa Kuwafundisha Watoto Mambo ya Utaifa

Katika mahojiano na mwandishi, sababu mojawapo iliyobainika kuhusiana na msukumo wa kuandika vitabu hivyo vinne, tena kwa motifu ya utaifa, ni msukumo binafsi wa kuwafundisha watoto mambo ya utaifa. Mwandishi alidai kwamba, yeye kama mlezi na mtafiti, anawafahamu watoto wa Kitanzania na mahitaji yao kimalezi. Hivyo, katika ufuatiliaji wake aliona kuwa watoto wanahitaji kulelewa katika misingi ya kujitambua kuwa wametoka wapi, wako wapi ili waweze kujitabiria wapi wanaelekea.

---

[2] Kwa mujibu wa mahojiano ya tarehe 30/01/2017 kati yangu na Prof. Mulokozi (mwandishi wa vitabu teule)

[3] *Kama hapo juu*

Pia, hoja ya Mulokozi niliyoieleza hapo juu inabainika wazi katika sehemu ya *Chanzo* katika *Moto wa Mianzi* (kur. vi-vii). Tena, katika tabaruku na dibaji ya kitabu cha *Utenzi wa Nyakiiru Kibi* mwandishi anaeleza kwamba watoto wa Kitanzania hawajui ya kwao na hivyo ipo haja ya kuwaandikia ili wajue walitokea wapi, wahenga wao walifanya nini, na zipi tunu za taifa ambazo zinapaswa kutunzwa bila kushikwa na kutu katika nyakati zote. Mwandishi anasema "Utenzi natabaruku, kwa wana wa nchi yetu, vijana wa hizi siku, wasiojua ya kwetu. Someni msiyasahau, mambo ya wahenga wetu, ni kweli wala si chuku, ni tunu ya watu wetu" (taz. tabaruku ya *Utenzi wa Nyakiiru Kibi*).

Uchambuzi na Mjadala

Kwanza kabisa, uchambuzi wa data unaonesha kwamba dhana ya utaifa imesisitizwa sana na kwa kurudiwa na mwandishi katika vitabu vyake vyote. Mwandishi anakiri kwamba ipo haja ya dhana hii ya utaifa kuendelea kujengwa na kukarabatiwa kila siku hasa katika bongo za watoto na vijana. Tena, "inafahamika kwa kila mtu kwamba ujenzi wa dhana kwenye bongo ya mtu [mathalani kuhusiana na masuala ya utaifa] hufanikiwa zaidi kwa mtu huyo akiwa bado mtoto/kijana" (Nyerere, 1968: 228). Bunilizi hizi za kihistoria, zina umuhimu mkubwa wa kuwapa maarifa, kuwaasa na kuwakumbusha wanajamii (hasa watoto wanaosoma bunilizi hizo) historia muhimu ambayo huwafanya wajione kuwa kitu kimoja na wajivunie taifa lao mara zote kutokana na kuwa na historia inayowagusa wote ikiwashawishi kuendelea kuwa wamoja.

Pili, hoja yangu ya hapo juu inashabihiana na ukweli kwamba malezi ya watoto katika jamii ni muhimu sana kwa ujenzi wa taifa endelevu na imara. Watoto wakikosa malezi huenda baadaye wakaja kuwa watu wasio na mwelekeo mzuri katika maisha yao wenyewe na taifa kwa ujumla. Katika ujenzi wa taifa, mtoto ni mali ya watu wote. Kila mmoja katika jamii anapomwona mtoto akikosa, anapaswa kumrekebisha. Hivyo, kila mtu ana jukumu la kumpa malezi mazuri mtoto kwa faida ya wanajamii wote na si kuwaachia wazazi wa watoto peke yao. Ukweli huu ndio uliomsukuma Mulokozi kuandika kazi teule kwa sababu yeye ni mdau wa umoja wa kitaifa na anaamini kwamba watoto ni walengwa muhimu.

Tatu, data zinaonyesha kwambakatika ujenzi wa taifa lolote, mashujaa ni watu muhimu sana katika kujitoa na kuitumikia jamii kwa faida ya wengi. Mashujaa ni "watu wenye moyo thabiti ambao wanaweza kukabili mambo, hata kama ni ya hatari" (TUKI, 2013: 509). Vitabu vyote vilivyochambuliwa vina dhamira hii ya ushujaa ambao una faida sana kwa jamii. Ingawa tumezoea kuwa mashujaa ni watu maarufu na wakubwa, katika vitabu hivi mashujaa wako mchanganyiko. Mashujaa wengi ni watoto na wachache ni watu wazima. Hivyo, vitabu vya kuwajengea watoto moyo wa kishujaa bado vinahitajika na ni muhimu.

Nne, katika kazi teule za Mulokozi, historia na urithi wa jamii yanaonekana kuwa mambo ya msingi katika kusisitiza dhana ya utaifa. Historia na urithi wa taifa ni mambo muhimu sana katika kujenga umoja na mshikamano katika nchi. Anderson

(2006) anasisitiza kwamba historia na urithi wa taifa huwafanya watu wajione kuwa wamoja kwa sababu ya kuwa na vinasaba vinavyowahusu wote huko nyuma. Umuhimu huu ndio unawafanya wafuasi wa nadharia ya Uoniafrika kushadidia kwamba ili kuzielewa jamii za Kiafrika lazima kujikita katika historia za jamii husika (Asante, 1998).

Tano, katika fasihi ya Kiswahili, wataalamu (taz. Mulokozi, 1990; 1996; 2012; Traore, 2010, 2011; Mlaga, 2011; 2013; 2015) wanaeleza kuwa bunilizi za kihistoria ni chache sana. Uchambuzi wa data unaonyesha kwamba uandishi wa kazi teule nne zilizorejelewa katika makala haya ulilenga kuendeleza bunilizi za kihistoria katika fasihi ya Kiswahili kutokana na uchache wa kazi hizi muhimu kwa watoto. Pamoja na juhudi hizi za Mulokozi, bado bunilizi za kihistoria, hasa zinazowahusu watoto ni chache sana. Mambo ya kujiuliza ni kwamba je, mpaka sasa kwa nini maendeleo ya aina hii adimu ya fasihi yamedumaa? Je, jamii ya waandishi haijui umuhimu wa bunilizi hizi kwa watoto? Je, kazi hizi ni ngumu kuandaa tofauti na kazi nyingine za fasihi? Serikali na vyombo vyake vinavyoshughulikia elimu ya watoto wa Kitanzania, wanafahamu umuhimu wa aina hii ya fasihi katika kuwajenga watoto katika dhana ya utaifa? Pengine, kukosekana kwa majibu ya maswali hayo ndiko kunakoendelea kudumaza aina hii ya fasihi muhimu kwa watoto. Aidha, majibu ya maswali niliyouliza hapo juu bado yanahitaji utafiti wa kina nje ya mjadala wa makala haya.

Sita, katika mataifa karibu yote duniani, kila serikali, hasa ya kidemokrasia, inayoingia madarakani hujinadi kuwa na ajenda ya kuhakikisha kwamba taifa linakuwa na umoja na mshikamano ili nchi iweze kupata maendeleo ya haraka. Hii inaonyesha ni kwa kiasi gani ajenda ya ujenzi wa taifa ni endelevu katika kila taifa. Kwa mujibu wa wataalamu wa fasihi (taz. Chinweizu, 1987; Amuta, 1989; Memmi, 2006; Lehman, 2006), nafasi ya fasihi katika ajenda ya ujenzi wa taifa ni kubwa. Mathalani, Chinweizu (1987) anabainisha kwamba fasihi inashiriki kwa kiasi kikubwa katika ujenzi wa taifa kwa kufanya haya yafuatayo: Mosi, kwa kuunga mkono malengo mazuri na kuangaza mustakabali mzuri wa taifa kwa sababu mawazo na hisia za watu katika taifa zinatakiwa kuthaminiwa kadri iwezekanavyo. Pili, fasihi husisitiza kutathmini uelewa sahihi wa wananchi. Kama wananchi wana mtazamo au fikra potofu, fasihi huwajuza kuhusiana na hali hiyo na hivyo kuweka kioo mbele yao ili wanajamii wajitazame kuhusiana na mienendo yao kimaisha na kijamii. Tatu, fasihi husaidia katika kuchunguza fursa zilizopo katika ujenzi wa taifa. Katika hili, fasihi husaidia katika kutoa mwelekeo mzuri wa taifa na maisha yatakavyokuwa katika taifa hilo, na kadhalika. Hivyo, Mulokozi anaonekana kuungana na wataalamu hao wa fasihi kwa kuamini kwamba kazi za fasihi, zinaweza kuwajengea dhana msingi na muhimu watoto kuhusiana na masuala ya utaifa.

Saba, kama wanavyosisitiza akina Achebe (1976) na Chinweizu (1987), mwandishi wa Kiafrika anapaswa kuwa mwalimu wa jamii yake. Mwandishi wa fasihi, tena fasihi ya watoto kama alivyofanya Mulokozi, anatarajiwa kuwa mwalimu na mlezi wa watoto. Maelezo ya mwandishi yanaonesha kwa uwazi kwamba yeye anakubaliana na ukweli kwamba waandishi wa fasihi wakati mwingine wanaweza kuisaidia serikali

iliyoko madarakani katika ajenda ya ujenzi wa dhana ya utaifa kwa wananchi wake, hasa watoto. Mawazo haya yanachukuana na yale ya Nadharia ya Uoniafrika kwamba mwandishi ni mwalimu, mwelekezi na mdau mkubwa wa kuipa jamii mwelekeo mzuri.

Hitimisho

Makala yamechambua bunilizi teule kwa nia ya kuchunguza motifu ya utaifa na sababu za mwandishi kuitumia motifu hiyo. Bunilizi hizi za kihistoria kwa ajili ya watoto zinaonekana kuwa muhimu sana ingawa umuhimu wa utafiti na uandishi wa bunilizi hizi haujaangaziwa vyema nchini Tanzania. Kazi chache zilizochambuliwa zinaonyesha kwamba bunilizi za kihistoria zina mchango mkubwa katika ujenzi wa dhana ya utaifa kwa watoto. Wito wa makala haya ni kusisitiza juhudi zaidi ziendelee kuwekwa ili bunilizi za Kiswahili za kihistoria kwa ajili ya watoto ziandikwe kwa wingi kwa sababu zinawapa watoto maarifa ambayo ni adimu sana katika ulimwengu huu wa utandawazi. Katika ulimwengu huu wa utandawazi, njia nzuri ya kujifunza mambo ya zamani ni kupitia usomaji wa kazi andishi. Watoto hawana muda tena wa kukaa na wazee wao ili wasimuliwe mambo ya zamani.

Marejeleo

Mulokozi, M. M. 1997. *Utenzi wa Nyakiiru Kibi*. Morogoro: ECOL Publications.

Mulokozi, M.M. (1991). *Ngome ya Mianzi*. Dar es Salaam: MPB Enterprises.

Mulokozi, M. (1991). *Ngoma ya Mianzi*. Morogoro. ECOL Publications.

Mulokozi, M. (1996). *Moto wa Mianzi*. Morogoro. ECOL Publications.

Achebe, C. (1976). *Morning not yet on Creation Day*. New York: Anchor Books.

Achebe, C. (1990). *Hopes and Impediments: Selected Essays*. New York: Anchor Books.

Amuta, C. (1989). *The Theory of African Literature: Implications for Practical Criticism*. London and New Jersey: Institute of African Attractives, ZedBooks Ltd.

Anderson, B. (2006). *Imagined Communities*. London: Verso.

Asante, M.K. (1998). *The Afrocentric Idea (Revised and Expanded Edition)*. Philadelphia: Temple University Press.

Asante, M.K. (2003). *Afrocentricity: The Theory of Social Change (Revised and Expanded)*. Chicago, Illinois: African Images.

Chinwenizu. (1987). *Decolonizing the African Mind*. Lagos: Pero Press.

Cianciolo, P. (1981). Yesterday Comes Alive for Readers of Historical Fiction, *Language Arts*, *National Council of Teachers of English*, 58 (4): 452-462. [Mtandaoni] Inapatikana: http://www.jstor.org/stable/41961351 [2014, Desemba 6].

Jacobs, L.B. (1952). Some Observations on Children's Historical Fiction,*Elementary English*, 29 (4) 185-189. [Mtandaoni] inapatikana:http://www.jstor.org/stable/41383936 [2014, Desemba 6].

Jacobs, L.B. (1961). Historical Fiction for Children, *The Reading Teacher*, *Explorations in Reading Research*, 14 (3) 191-194. [Mtandaoni] inapatikana: http://www.jstor.org/stable/20197363 [2014, Desemba 6].

Kimbi, G. (2016). Dhima ya Takriri ya Kidhamira katika Riwaya za Watoto za Mulokozi. Tasnifu ya Umahiri katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).

Köksal, D. (2001). Fine-Tuning Nationalism: Critical Perspectives from Republican Literature in Turkey, *Turkish Studies*, 2 (2): 63-84. [Mtandaoni] inapatikana: http://dx.doi.org/10.1080/714005687 [2016, Mei 7].

Lehman, B.A. (2006). Children's Literature and National Identity in the New South Africa, *Sankofa*: *A Journal of African Children's and Young Adult Literature,* (5) 6-20.

Memmi, A. (2006). *Decolonization and the Decolonized*, translated by Roberto Bononno. London: University of Minnesota Press.

Mlaga, W. (2011). Historia ya Tanzania Kuanzia Miaka ya 1960 hadi 1980 Inavyosawiriwa Katika Riwaya Teule: Uhakiki wa Kihalisia. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).

Mlaga, W. (2013). Riwaya ya Kiswahili katika Ufundishaji wa Historia, *Kiswahili*, 76: 29-44.

Mlaga, W. (2015). Uhistoria katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka Riwaya ya *Ndoto ya Ndaria*, *Gamba la Nyoka* na *Miradi Bubu ya Wazalendo*, *Kiswahili,* 78: 23-37.

Mulokozi, M. (1990). Utunzi wa Riwaya ya Historia, *Mulika* (22): 1-10.

Mulokozi, M. M. (1996).*Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili.*Dar es Salaam: KAUTTU.

Mulokozi, M.M. (2012). *Makuadi wa Soko Huria* (Chachage S. Chachage) katika Muktadha wa Riwaya ya Kihistoria katika Fasihi ya Kiswahili, *Mulika* (31): 51-66.

Mushengyezi, A. (2003). *Twentieth Century Literary Theory*. Kampala: Mukono Publishing Company Ltd.

Musiyiwa, M. (2008). The Significance of Myth and Legends in Children's Literature in Contemporary Zimbabwe. Makala iliyowasilishwa katika *The 31st IBBY Congress, Copenhagen* [Mtandaoni] inapatikana: www.ibby.org/913.0.html [2017 Agosti 30].

Muwati, I., Gwekwerere. T, na Gambahaya, Z. (2010). Children's Literature, Child Engeneering and the Search for an Ennobling Gender Paradigm, *Zimbabwe Journal of Educational Reasearch*, 22 (2): 202-214.

Ntarangwi, M. (2004). Uhakiki wa Kazi za Fasihi. Tasnifu ya Uzamivu, Augustana College, Rock Island (Haijachapishwa).

Nyamsenda, J.C. (2015). Ushujaa wa Shujaa wa Motifu za Mafari na Msako katika Ngano za Waikizu, Wabondei na Wazanzibari. Tasnifu ya Uzamivu ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Haijachapishwa).

Nyerere, J.K. (1968). The Power of Teachers, in *Freedom and Socialism [Uhuru na Ujamaa]: A Selection from Writing and Speeches 1965-1967*: 223-228. Dar es Salaam/Nairobi/London/New York: Oxford University Press.

Okofor, V.O. (2010). Understanding the Afrocentric Conceptual Paradigm, katika Robertson, C.C. (mh.). *Africa Rising: Multidisciplinary Discussion on African Studies and History*. Asmara: Africa World Prss, Inc. kur.11-24.

Okpehwo, I. (1992). *African Oral Literature. Backgrounds, Character, and Continuity.*Bloomington: Indiana University Press.

Oxford University Press. (2015). *Oxford Advanced Learner's Dictionary: International Student's Edition* (9th Edition). Great Clarendon Street, Oxford: Oxford University Press.

Rycik, M.T. na B. Rosier. (2009). "The Return of Historical Fiction" *The Reading Teacher*, 2:163-166: [Mtandaoni] Inapatikana http://www.jstor.org/stable/40347667 [2014 Desemba 6].

Senkoro, F.E.M.K. (2011). *Fasihi*.Dar es Salaam: KAUTTU.

Traore, F. A. (2010). Swahili Children's Literature in Contemporary Tanzania. *Journal des africanistes*:80 (1-2) 176-191. [Mtandaoni] inapatikana:http://africanistes.revues.org [2016, Mei 4].

Traore, F.A. (2011). Children's Literature in African Languages: Kiswahili Books for Children in Kenya and Tanzania. Makala iliyowasilishwa katika *The Fourth European Conference on African Studies.*Tarehe 15-18 Juni, Chuo Kikuu cha Uppsala, Sweden.

TUKI. (2013).*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la Tatu). Dar es Salaam/Nairobi: TUKI/Oxford University Press.

Wamitila, K. W. (2003).*Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.